


# Ushairi na Utamaduni:

## Natija na Mawanda yake katika Tungo za Wamvita


Na

***Ahmed Hussein Ahmed***

Pwani University22

# Utangulizi 1.0

Ushairi ni nini? Hili ni swali ambalo lataka uyakinifu kulijibu. Twasema hivyo kwa sababu kuna tetesi za wanaojiita wanamapinduzi wa ushairi; nao wanaodai kuwa; "*Ushairi ni mtiririko wa mawazo yenye kuilimisha au kupumbaza jamii na ati hapana lazima ya kufuata arudhi*". Yaani mawazo hayo si lazima yawe yatafuata kanuni za kuchunga mizani na vina. Sisi tuitwao wana hafidhina twasema "La! La! *Hashaa wa kalla*!" Ushairi si kupanga misitari ya maneno au kuandika barua. Mimi naona watu hao kama hawawezi kutunga mashairi ni afadhali waandike riwaya au tamthilia kueleza mawazo yao. Kwani mashairi ya kale yalikuwa na vina ijapokuwa mengineyo hayakuwa na sharti la kuandamisha mizani. Kwa mfano;

***BIBI SONGA NYWELE***

*Bibi songa nywele, Shanuo la nini?*
*Kichwa chaniuma, Dawa yake n'nini?*
*Ponda tangawizi upake nyusini,*

Huu ni wimbo wa kale sana na pngine wengi wameusahau. Utunzi huu unaonyesha mtiririko wa vina unapatikana. Ushairi wa Kiswahili, tabaani, una misingi yake. Una kunga zake, chambilecho wengine wanaita *arudhi*. Kwa ufupi, katika hutuba hii tutaeleza

# Usuli wa Mada 2.0

Kwa karne na kuruni mashairi yalikuwa yakighaniwa kwa malengo mbali mbali. Mashairi ni sehemu ya utamaduni wa Waswahili. Waswahili wenyewe wanajieleza na kueleza mambo yao kwa kutumia tungo. Maelezo yafuatayo yanatupa pepe pepe za mawanda haya ya kujieleza kishairi.

**2.1 Kuelimisha**

Ushairi unaweza kutolewa kwa lengo la kuelimisha. Kuelimisha huku kuna uvutio mno. Kwa mfano;

***ELIMU KITU AZIZI***

*Negema ewe twalibu, mtukufu mwanafunzi,*

*Mwenye twaa na adabu, kwa kila mtu mpenzi,*

*Fungua hicho kitabu, ukisome kwa henezi,*

*Elimu kitu azizi, kisoma hupati tabu.*

**2.2 Kufurahisha**

Mshairi pia anaweza kutunga mashairi kwa lengo la kufurahisha wasikilizaji wake. Kwa mfano Muyaka anatongoa;

*Niwene shundwa na mbuzi, wachandamana pamoya,*

*Na kuku mke na kozi, wanawao wachileya,*

*Na mtu msimaozi, achionya watu ndiya,*

*Hayano sikuambiwa, nimeyaona wenyewe.*

**2.3 Ushairi wa Unyumba**

Kuna mashairi ambayo yanatungwa kwa lengo la kueleza mas'ala ya unyumba au yaliyo baina mume na mke. Kwa mfano Muyaka anasema;

*Nimeuja pasi tumi, nijile kupulikiza,*

*Ulilonalo husemi, mno lingakutatiza,*

*Na nikuambialo mimi, hutaki kunisikiza,*

*Sinifanyie mayaza, kana hutaki nambia.*

**2.4 Ushairi Hukuza Lugha**

Kuna mashairi mengi ambayo yametungwa kwa lengo hili. Washairi wengi wanahafidhina wametunga kufunza watu lugha. Katika kadhia hii pia wanaonyesha ukwasi wa lugha. Kwa mfano;

***PANDA***

*Panda uangushe nazi, zile zinazobembea,*

*Panda kunde na mbaazi, huku ukipalilia,*

*Panda ndege mandakozi, uruke naye badia,*

*Panda kisha ukijua, kuna na kushuka ngazi.*

***METHALI***

*Mbona umekuja resi, pasi na hodi kugonga?*

*Ukanikopa fulusi, nikakupa ja mchanga,*

*Kumbe kukopa harusi, kunilipa ni matanga!*

*Wapenda kujipa kazi, ikakushinda njiani,*

*Hebu toka ujingani, tuza bongo kwa makini,*

*Farasi hamuwawezi, ndovu mutawalishani?*

**2.5 Ushairi Huhifadhi Lahaja/Lugha**

Ushairi pia ulinufaisha wengi kwa kuhifadhi lugha, maneno ya kale na lahaja zetu. Kwa mfano kuna shairi amabalo nimelitunga kwa lengo ya kukumbusha maneno Fulani yaliyosahaulika. Maneno haya yalikuwa katika michezo ya watoto nyakati za nyuma hapa Mvita.

***GOLOLI***

*Twalikiteza gololi, Mvita na Mringwari,*

*King'oto watu wawili, akitunyuta hodari,*

*Tena huzibanja nguli, gwanyu hukosa uzuri,*

*Sharuti uzibadili, kama hizo hazingari,*

*Mbirisau si gololi, bunta is kiporo poro.*

**2.6 Ushairi Hutumiwa Katika Kushindana na Kuimbana Kishairi**

Washairi wanajulikana kwa kuimbana na kulumbana kishairi. Aghalabu huimbana na kujibazana kwa kutunga mashairi papo kwa papo. Kwa mfano;

**Mashairi ya Kufunga Nyama**

**SHAHA WA KWANZA:**

*Watafunaji azizi, kitarazaki kanwani,*

*Nanyi wenye vikohozi, na mutemao ndiani,*

*Nipani khabari hizi, nipate kujimakini,*

*Nambiyani kitu gani, kisotemwa kisomizwa?*

**SHAHA WA PILI:**

*Umetuuliza swali, watemi na watafuni,*

*Mwinani sijithakili, takutoa ujingani,*

*Lako jibu twaa hili, pulika ujimakini,*

*Ni 'ULIMI' mdomoni, usotemwa usomizwa*

**2.7 Vitendawili**

Ushairi piya waweza kumpa mtu ufasaha wa kauli na ukuzo wa akili. Kwa mfano;

***HUVUSHWAJE DAU MOJA?***

*Napenda kukuuliza, kufunga nyama amiri,*

*Wafuga lawashangaza, wawinda huwashamiri,*

*Tafadhali nieleza, uwaze ukifikiri,*

*Chui, manyasi na mbuzi, huvushwaje dau moja?*

**2.8 Utenzi**

Ushairi unaeleza jamii, visa, khabari zinazotuka, kusifu na kutoa hekaya. Maelezo haya huelezeka kwa njia nyepesi ya Utenzi. Kwa mfano;

**UTENZI WA KIJANA MRONGO**

1. *Changu kisa na maana,*
   *Chahusu mmoja mwana,*
   *Aliyepewa dhamana,*
   *Mifugo kuichungiya.*

2. *Wakanena hao watu,*
   *Chunga kijana wetu,*
   *Na akija mbwa mwitu,*
   *Hima mbiu tupigiya.*

3. *Kasema hilo rahisi,*
   *Mifugo kulisha nyasi,*
   *Atawaita upesi,*
   *Mbwa mwitu kitokeya.*

4. *Akashika lake gongo,*
   *Akapanga urongo,*
   *Mara akapiga pigo,*
   *owe kubwa akatowa.*

5. *Watu waliposikiya,*
   *Huyo kijana aliya,*
   *Mbio walizitimua,*
   *Wapate msaidiya.*

### *2.9* Kujigamba Kishairi

Washairi pia wanapenda kujigamba kishairi. Mfano mzuri ni yale majigambo au majitapo ya Malenga wa Mvita alipotoṫorwa na kuambiwa;

Malenga wa Amu( atongoa):

"*Ewe baba uvuae, maji yamezongamana,*

*Mshipi wako utoe, ubadilishe ndoana,*

*Hapo pana mai toe, samaki wakubwa sana.*

*Na mshipi fupilisha, usiwe mrefu sana,*

*Na chambo kibatilisha, utie chambo cha una,*

*Ndipo watakapolisha, uwavute wakiona."*

Malenga wa Mvita (ajibu):

*"Ndimi mvuvi halisi, kula vuvi nalijuwa,*

*Nivuae mikambisi, na papa wenye khatuwa,*

*Wala sivui vingisi, mishipi kuisumbua,*

*Nimekwambiya elewa."*

Kwa mukhtasari, kuna aina nyingi za tungo zinazolenga jamii na utamaduni wake. Mshairi anaeleza jamii yake, mazingira yake na hujieleza mwenyewe. Hutunga maneno kwa ufasaha na ustadi. Hujieleza kwa uvutio na kufahamika kwa urahisi.

# Hitimisho 3.0

Katika mada yetu tumetazama ushairi wa wanahafidhina na jinsi washairi wanajieleza na kuieleza jamii yao. Ni vigumu kuuvua ushairi wetu kutoka kwa utamaduni wetu. Natija zinazopatikana ni nyingi. Kwa mfano kuilimisha, kuhifadhi lugha, kuonya, kusherehekea jambo, na kujigamba.

# Marejeleo


Abdalla, A (1978) *Sauti ya Dhiki*, Oxford University Press; Nairobi.

AbdulAziz, M (1979) *Muyaka*, Kenya Literature Bureau; Nairobi.

Ahmed, A H (1998) "*Malumbo ya wa-Mvita*" makala kutka jarida la JUA,; Cologne.

Nassir, A (1971) *Malenga wa Mvita*, Oxford University Press; Nairobi.

Sharif na Blersker (1955) *Mashairi ya Vita vya Kuduhu*, Michigan State Univ. Press, E Lousing.